



# ISEMAVYO SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA, 2017

**KIMEANDALIWA NA MTANDAO WA MASHIRIKA  
YANAYOTOA MSAADA WA KISHERIA (TANLAP)  
KWA KUSHIRIKIANA NA WIZARA YA MAMBO YA  
KATIBA NA SHERIA**

**Waandishi**

Bi. Christina Kamili Ruhinda

Bw. Pasience Mlowe

Wakili Esta Msambazi

Wakili George Mollel

Wakili Gideon Mandesi

**Bodi ya Uhariri**

Dr. Helen Kijo-Bisimba

Bi. Felistas Mushi

**Kimefadhiliwa na USAID na Ubalozi wa Finland**



**USAID**  
KWA HISANI YA WATU  
WA MAREKANI



**MINISTRY FOR FOREIGN  
AFFAIRS OF FINLAND**

**Yaliyomo**

1.0	UTANGULIZI.....	1
2.0	KUHUSU KIJARIDA HIKI .....	1
3.0	SEHEMU YA KWANZA.....	2
4.0	SEHEMU YA PILI: UANZISHWAJI WA VYOMBO VYA URATIBU.....	3
5.0	SEHEMU YA TATU: USAJILI WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA.....	6
6.0	SEHEMU YA TANO: .....	11
6.1	UTOAJI WA MSAADA WA KISHERIA .....	11
6.2	MSAADA WA KISHERIA KWENYE MASHAURI YA MADAI .....	12
6.3	HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA KWENYE MASHAURI YA JINAI.....	14
7.0	MASHARTI MENGINEYO.....	15
8.0	HITIMISHO.....	18



### **1.0 UTANGULIZI**

Mtandao wa mashirika ya watoa huduma ya msaada wa kisheria Tanzania (TANLAP) ni mtandao wa kitaifa unaofanya kazi katika sekta ya sheria na hususan msaada wa kisheria. Mtandao huu unajumuisha mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), mashirika ya kijamii (CBOs), mashirika ya kiimani (FBOs) na taasisi nyingine zinazotoa msaada wa kisheria nchini Tanzania. Mtandao huu ulianzishwa mwaka 2006, ukiwa na lengo kuu la kufanya kazi na kuunganisha mashirika mengine ya kiraia ili kuhakikisha utoaji bora wa msaada wa kisheria na kutetea upatikanaji wa haki miongoni mwa watu maskini na wanyonge nchini Tanzania.

### **2.0 KUHUSU KIJARIDA HIKI**

Kijarida hiki kinahusu Sheria ya Msaada wa Sheria, namba 1 ya mwaka 2017 ambayo inatumika Tanzania bara peke yake. Sheria hii ina malengo ya kuwatambua wasaidizi wa kisheria, kuboresha utoaji wa msaada wa sheria na kufuta sheria ya Msaada wa Sheria (Makosa ya Jinai) Sura namba 21. Uandalizi wa kijarida hiki umekuwa shirikishi ambapo mashirika mbalimbali yanayotoa msaada wa sheria na wadau muhimu kutoka serikalini wanaohusika na huduma za sheria wameshiriki katika mchakato wa kuichambua na kuiweka katika lugha rahisi. Madhumuni ni kuwasaidia watoa huduma ya msaada wa kisheria kote nchini kuweza kuielewa sheria hii ili kuongeza ufanisi katika kuitumia kuwahudumia wanajamii. Pia, kinatarajiwa kutumiwa nawahitaji wa huduma hiyo ili waweze kudai huduma bora na stahiki kwa mujibu wa masharti ya sheria hii.

Chimbuko la sheria hii lilitokana na uhitaji mkubwa wa kuwa na sheria nchini itakayoongoza kisheria namna ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wahitaji ili waweze kufikia haki. Sheria hii ilitungwa na bunge mnamo tarehe 31 Januari, 2017, ikapitishwa rasmi na kusainiwa na mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 21 Februari, 2017. Ilitanganzwa kwenye gazeti serikali namba 9 la 2017 na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2017 kwa mujibu wa tangazo la serikali namba 20 la mwaka 2017. Pia sheria hii imetungwa kukidhi matakwa ya mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo nchi yetu imesaini na kuridhia kuhusu haki za binadamu ikiwemo haki ya kupata msaada wa kisheria.

### 3.0 SEHEMU YA KWANZA

Sehemu hii ya kwanza inatoa tafsiri ya maneno muhimu yalitumika kwenye sheria. Hivyo basi kwa madhumuni ya kijarida hiki maneno machache yametolewa maana kama ifuatavyo:-

- *“Mtu anayesaidiwa”* maana yake ni mtu anayepatiwa msaada wa kisheria chini ya sheria hii.
- *“Mtu asiye na uwezo”* Maana yake mtu asiye na uwezo wa kumudu gharama za wakili wa kujitegemea ikiwa ni pamoja na makundi mengine ya watu kama itakavyohitajika kwa maslahi ya utoaji haki.
- *“Ushauri wa Msaada wa kisheria”* Maana yake ni ushauri na msaada unaotolewa kwa mtu asiye na uwezo katika mashauri ya jinai na madai kuhusu sheria husika, taratibu za kisheria na uandaaji wa nyaraka za kisheria.

- “Msaada wa kisheiria” au “huduma ya msaada wa kisheria” inajumuisha utoaji wa ushauri wa kisheria, usaidizi wa kisheria au uwakilishi kwa watu wasiokuwa na uwezo.
- “Mtoa huduma wa msaada wa kisheria” Maana yake ni taasisi iliyosajiliwa chini ya sheria hii kutoa huduma ya msaada wa kisheria.

### **4.0 SEHEMU YA PILI: UANZISHWAJI WA VYOMBO VYA URATIBU**

Sheria hii imeanzisha vyombo viwili vya uratibu.

- (a) Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Msaada wa kisheria ambayo inaundwa na wajumbe wafuatao kwa kuzingatia uwakilishi wa kijinsia. Muda wa kukaa madarakani kwa wajumbe wa bodi itakuwa miaka mitatu lakini wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu tu.
- o Mwenyekiti ambaye ni Jaji wa mahakama kuu ya Tanzania atakayeteuliwa na waziri husika akisaidiana na Jaji Mkuu
  - o Mwanasheria Mkuu au mwakilishi wake mwenye cheo si cha chini ya Afisa Sheria
  - o Mwakilishi mmoja kutoka jukwaa la taifa la haki jinai
  - o Mwakilishi mmoja kutoka Chama cha Mawakili wa kujitegemea Tanganyika
  - o Mkurugenzi wa huduma za sheria kutoka wizara inayohusika na tawala za mikoa na serikali za mitaa au mwakilishi wake

- o Mwakilishi wa watu wanaoishi na ulemavu
- o Mwakilishi mmoja kutoka taasisi zinazowakilishi wasaidizi wa kisheria
- o Katibu wa Bodi ya taifa ya ushauri wa msaada wa sheria atakuwa ni msajili

Miongoni mwa majukumu ya bodi, Kutoa miongozo ya kisera, kutoa ushauri, Kupitisha ripoti za mwaka za watoa huduma ya msaada wa sheria na kupokea na kutoa maamuzi ya rufani zitakazo pitia maamuzi ya msajili wa watoa huduma za msaada wakisheria.

- (b) Ofisi ya msajili wa watoa huduma wa msaada wa kisheria.
- (c) Katika ngazi ya taifa kutakuwa na msajili na katika ngazi ya wilaya na mkoa kutakuwa na wasajili wasaidizi. Miongoni mwa kazi zao itakuwa ni pamoja na; Kusajili watoa huduma wa msaada wa kisheria, Kuchunguza malalamiko yote yanayohusiana na watoa huduma ya msaada wa kisheria, Kusimamisha au kufuta usajili wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria, kutunza kumbukumbu ya orodha ya watoa huduma ya msaada wa kisheria, Kukagua ofisi za watoa huduma ya msaada wa kisheria ikiwa ni pamoja na kujiridhisha na aina na ubora wa huduma zitolewazo, kutoa elimu ya sheria na ufahamu miongoni mwa wanajamii, aidha, wataratibu na kuwezesha utayarishaji wa mitaala ya kufundishia wasaidizi wa kisheria kwa kushirikisha wadau muhimu.



Piaofisi hizi zitahusika na ufuatilia na tathmini ya kazi za utoaji huduma za msaada wa kisheria nchini na kutoa mapendekezo muhimu kwa ajili ya uboreshaji wake, kuweka kumbukumbu na kutatua migogoro baina ya watoa huduma ya msaada wa sheria isipokuwa mawakili na kutatua migogoro baina ya watoa huduma wa msaada wa kisheria na wateja; na kazi nyingine zitakazoelekezwa na Bodi

Katibu mkuuwa wizara ya Katiba na Sheria ndio ana mamlaka ya kuteua wasajili wasaidizi miongoni mwa watumishi wa umma ili kurahisisha usajili wa watoa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi za mkoa na wilaya ambao watawajibika kwa msajili. Watakuwawana jukumu la kusajili watoa huduma za msaada wa kisheria na kutoa vyeti vya usajili kwa niaba ya msajili isipokuwa hawatakuwa na mamlaka ya usajili wa taasisi inayoomba kutoa huduma zaidi ya mkoa au wilaya husika.

Fedha za kuendesha shughuli za Bodi hii zitatokana na vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja kiwango chochote kitakachotengwa na bunge na fedha zozote zitokanazo na michango au msaada uliopatikana ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyanzo vingine vitokanavyo na shughuli za bodi kama vile tozo, msaada au vyanzo vingine.

## **5.0 SEHEMU YA TATU: USAJILI WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA**

Kwa mujibu wa masharti ya sheria hii watoa msaada wa sheria ni lazima wasajiliwe. Msajili atawajibika kupeleka orodha yao katika taasisi za utoaji haki kama vile Mahakamani, Polisi na Magerezani. Hivyo basi ili kupata usajili taasisi itapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

1. Iwe imesajiliwa chini ya sheria husika
2. Utoaji wa wa huduma ya msaada wa kisheria ni moja ya majukumu yake ya msingi.
3. Ina ofisi na vifaa
4. Ina ama;
  - i. Mwakili wawili
  - ii. Wakili mmoja na mwanasheria mmoja
  - iii. Mwanasheria mmoja na wasaidizi wa kisheria wawili
  - iv. Wakili mmoja na wasaidizi wa kisheria wawili
  - v. Wasaidizi wa kisheria watatu;
  - vi. Na iwe na hati safi ya taarifa za kifedha.

Hata hivyo taasisi isiyo na wakili itapaswa kuwasilisha uthibitisho kwamba iko chini ya uangalizi wa Taasisi ya mtoa huduma za kisheria mwenye wakili.

Mambo muhimu yanayopaswa kuambatanishwa na maombi ya usajili kwa msajili au msajili msaidizi ni pamoja na:-

- a. Nakala ya Katiba ya taasisi au nyaraka iliyoanzisha taasisi
- b. Taarifa binafsi za wenye ofisi, mawakili au wasaidizi wa kisheria
- c. Anuani na mahali yalipo makao makuu ya taasisi.
- d. Nakala ya hati safi kutoka mamlaka ya usajili wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria.
- e. Ada ya usajili.
- f. Taarifa nyingine kama ambavyo itahitajika na msajili.

Hati ya usajili itatolewa baada ya usajili kukamilika ndani ya muda usiopungua siku ishirini na moja. Endapo maombi yatakataliwa mleta maombi atajulishwa ndani ya siku kumi na nne na sababu za kukataliwa zitabainishwa. Miongoni mwa sababu hizo za kukataliwa ni pamoja na, Kutotimiza masharti yaliyoanishwa katika masharti ya usajili na Kutoa taarifa za uongo au upotoshwaji.

Sheria pia inabainisha na kuweka taratibu za kusitisha au kufuta hati ya usajili endapo yafuatayo yatabainika; kukiuka maadili ya kitaaluma au kushindwa kumchukulia hatua za kinidhamu mwajiriwa aliyetenda kosa kinyume cha masharti ya sheria hii, kukiuka kanuni za maadili zilizowekwa, kutotii katiba iliyoanzisha taasisi husika na kutotunza kumbukumbu za shughuli za utoaji wa msaada wa kisheria zinazoathiri maslahi ya mtu anayesaidiwa kufikia haki yake. Na msajili kujiridhisha kwamba kuna athiri maslahi watu wanaosaidiwa.

Vilevile sababu nyingine zinazoweza kusababisha msajili kufuta hati ya usajili ni pamoja;

- a. Usajili umepatikana kimakosa, kwa udanganyifu, kwa ujanja, kwa ushawishi usio halali au kwa taarifa ya kupotosha.
- b. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria ameshindwa kutimiza masharti ya usajili.
- c. Sifa za kusajiliwa zimekoma.
- d. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria ametangazwa kufilisika.
- e. Wakili au msaidizi wa kisheria aliyeajiriwa na mtoa msaada wa kisheria amekuwa akikiuka mara kwa mara maadili ya kitaaluma.
- f. Mtoa msaada wa kisheria amembagua mteja kwa misingi ya dini, jinsia, kabila, utaifa au kisiasa.
- g. Mtoa huduma ya msaada wa kisheria ametiwa hatiani kwa makosa yanayohusu ubadhirifu, uwajibikaji wake au amepewa amri chini ya chombo husika.
- h. Kushindwa kutoa huduma katika kiwango kilichowekwa.

Endapo mtoa huduma ya msaada wa kisheria hataridhika na maamuzi na uamuzi wa kusitisha au kufuta hati ya usajili anayo haki ya kukata rufaaa kupinga maamuzi yaliyofikiwa. Endapo maamuzi yamefanywa na msajili msaidizi atapaswa kukata rufaa kwa msajili, na ikiwa maamuzi yamefanywa na msajili rufaa itapelekwa kwenye Bodi ya Taifa ya Ushauri, na kama Bodi ndio imefanya uamuzi husika rufani itakatwa kwa Waziri husika, na pia maamuzi ya Waziri yanaweza kupigwa kwa kukata rufaa Mahakama kikuu ya Tanzania.

### **SEHEMU YA NNE: VIPENGELE MAALUMU KWA WASAIDIZI WA KISHERIA**

Msaidizi wa kisheria kwa mujibu wa masharti ya sheria hii atapaswa kuwa na sifa zifuatazo;

- a. Elimu ya Shahada yeyote kutoka taasisi inayotambulika isipokuwa shahada ya sheria.
- b. Elimu ya Stashada au astashahada yeyote kutoka taasisi za elimu na mafunzo zinazotambulika.
- c. Elimu Cheti cha sekondari.

Pamoja na sifa hizi msaidizi wa kisheria anapaswa kupata mafunzo mahususi ya wasaidizi wa kisheria. Pia sheria inatambua wasaidizi wa kisheria waliokwisha kupata mafunzo miaka miwili kabla ya kuanza kutumika kwa sheria.

Hivyo basi msaidizi wa kisheria anayetambulika katika sheria hii atakuwa na majukumu kama ifuatavyo;

- a. Kuendesha mafunzo kwa lugha ya Taifa au inayotumiwa na wenyeji wa eneo husika kuhusu masuala ya kisheria na taratibu zinazohusu jamii.
- b. Kumsaidia mteja kupata nyaraka mhimu za kisheria.
- c. Kumuelekeza mteja anayesaidiwa njia sahihi kupata haki yake.
- d. Kushauri pande zote zinazopingana na kutafuta suluhu ya mgogoro au kuwaelekeza kwenye vyombo vinavyohusika na utatuzi wa migogoro.

Sheria inakataza msaidizi wa kisheria kufanya kazi za wakili. Pia hapaswi kutoza gharama yeyote ya kitaalam kwa ajili ya huduma ya msaada wa kisheria aliyoitoa kwa mtu asiye na uwezo. Msaada wa kisheria utatulewa bure isipokuwa pale ambapo sheria itaelekeza tofauti, hata hivyo huduma haipaswi kuwa ya kiwango cha chini kwa kigezo cha kutolewa bure.

## **6.0 SEHEMU YA TANO:**

### **6.1 UTOAJI WA MSAADA WA KISHERIA**

Sheria hii imeweka masharti ya utaratibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa watu wanaosaidiwa. Hivyo anayehitaji kusaidiwa anapaswa kufanya maombi kwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria. Hivyo basi taasisi ya utoaji wa huduma za kisheria itaangalia sifa za mwombaji kulingana na taratibu za taasisi husika.

Maombi ya msaada wa kisheria yatafanywa na Mhitaji mwenyewe au mwakilishi wake aliyemteua au shirika kwa niaba ya mtu anayehitaji kusaidiwa ambaye hana uwezo wa kulipa gharama za mawakili wa kujitegemea.

Kwa masharti ya sheria hii msaada wa Kisheria utatolewa na taasisi tu ambayo imesajiliwa na sio watu binafsi. Hivyo basi mawakili, wanasheria na wasaidizi wa kisheria watatoa huduma ya msaada wa kisheria kwa niaba ya taasisi husika. Mtu yeyote atakayekiuka utaratibu uliowekwa nasheria kuhusiana na utoaji wa msaada kisheria kupitia taasisi atakuwa ametenda kosa na adhabu yake itakuwa faini ya shilingi milioni tano au kifungo cha mwaka mmoja jela au vyote viwili.

Pia mtu yeyote atakayetoza fedha kinyume na sheria atakuwa ametenda kosa na adhabu yake itakuwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kifungo kisichopungua miezi sita jela au vyote viwili. Pamoja na adhabu iliyotajwa hapo juu, mtu huyo atatakiwa pia kurejesha fedha alizochukua kwa mteja wake.

Mtoa huduma za msaada kisheria atawajibika kutoa msaada wa kisheria kwa minajili ya kulinda maslahi ya mtu anayesaidiwa na kutunza kumbukumbu ya shughuli zake. Na nakala ya kumbukumbu hizo itawasilishwa kwa msajili au msajili msaidizi kwa madhumuni ya ufuatiliaji na kufanya tathimini ya ubora wa huduma iliyotolewa katika kipindi cha mwaka husika.

## **6.2 MSAADA WA KISHERIA KWENYE MASHAURI YA MADAI**

Kwenye mashauri ya madai Jaji au hakimu au mwenyekiti wa baraza anaweza kutoa amri ya mtu asiyekuwa na uwezo wa kugharamia uwakilishi wa wakili, kupewa huduma ya msaada wa kisheria kutoka kwa mtoa huduma za msaada wa kisheria. Amri hiyo itatolewa kwa kuangalia mambo mawili;-Uwezo wa kifedha au Kwa maslahi ya upatikanaji wa haki.

Taarifa za shauri husika zitatolewa na mtoa huduma za msaada wa kisheria kwa upande mwingine kwenye mgogoro na kuitaarifu mahakama juu ya huduma hiyo. Pia endapo mtoa huduma ataamua kujiondoa au mteja ameamua kusitisha huduma ya kupokea msaada wa kisheria kutoka kwenye taasisi husika itatakiwa kuitaarifu mahakama na upande wa pili.

Endapo mtu anayesaidiwa atashinda kesi na amepewa tuzo na mahakama ya kulipwa gharama atakuwa anasthili kulipwa gharama baada ya Taasisi iliyotoa msaada wa kisheria kukata/ kuondoa sehemu ya gharama zake.



Kuhusu utekelezaji wa hukumu *“Taasisi inayotoa msaada wa kisheria itachukua hatua stahiki katika kutekeleza hukumu au makubaliano ili kutekelezwa kwa tuzo iliyotolewa”*

Sheria inasisitiza zaidi kwamba katika mashauri ya madai iwapo mtu anayesaidiwa atashindwa mahakama haitatoza gharama isipokuwa gharama zitatozwa katika mazingira maalumu yafuatayo;

- (a) Mwenendo uliofanywa na mteja uliopeleka upande wa pili kuingia gharama zisizokuwa za lazima.
- (b) Kukataa bila sababu za msingi utaratibu wa kufikia muafaka kwa shauri linalobishaniwa.
- (c) Vitendo vya upotoshaji na udanganyifu vilivyofanywa na mtu aliyesaidiwa msaada wa kisheria.
- (d) Matendo mengine yaliyofanywa na mtu aliyesaidiwa yaliyoathiri mchakato wa mahakama kwenye kufikia haki.
- (e) Taasisi iliyotoa msaada wa kisheria haitawajibika kulipa gharama zozote.

Sheria hii pia inamtaka mtu anayesaidiwa wakati wa uendeshaji wa shauri au rufaa, kutokupewa dhamana ya kitu chochote.

### **6.3 HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA KWENYE MASHAURI YA JINAI**

Katika mashauri ya jinai endapo itaonekana kuwa mtuhumiwa anahitaji msaada wa kisheria, Jaji au Hakimu akijiridhisha kuwa mtuhumiwa hana uwezo na ni kwa maslahi ya upatikanaji wa haki, anaweza kutoa amri kuwa mtuhumiwa husika apatiwe msaada wa kisheria. Msajili wa Mahakama Kuu atatakiwa kuteua Taasisi ya msaada wa kisheria yenye Wakili kwa lengo la kuandaa utetezi au rufaa ya mtuhumiwa.

Iwapo mtuhumiwa kwenye shauri la jinai ni mtoto, Jaji au Hakimu atatakiwa kuidhinisha kuwa mtuhumiwa anahitaji msaada wa kisheria na idhini hiyo ikishatolewa, Msajili atateua Wakili kwa ajili ya kuandaa utetezi wa shauri husika. Gharama za Wakili zitaidhinishwa na Jaji Mkuu kutoka kwenye mfuko wa mahakama.

Taasisi ya msaada wa kisheria iliyoteuliwa kumwakilisha mtuhumiwa ikiingia gharama za ziada inaweza kupeleka madai kwa mtendaji mkuu wa mahakama kwa ajili ya kurejeshewa gharama zake. Mtendaji Mkuu wa mahakama akijiridhisha na madai yaliyopelekwa kwake anaweza kulipa gharama zote au kiasi fulani cha madai. Endapo kutakuwepo na kutokukubaliana na malipo baina ya Taasisi na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, malalamiko yatapelekwa kwa Jaji Mkuu kwa ajili ya maamuzi ya mwisho. Jaji Mkuu, anaweza kukaimilisha kazi zake katika suala hili kwa njia ya maandishi kwa Jaji Kiongozi.

Endapo mtu yeyote anayeshughulika na ustawi wa watoto wakati wa utekelezaji wa kazi zake atakutana na shauri la mtoto aliye kwenye mgogoro na sheria, atafanya utaratibu wa mtoto husika kupata msaada wa kisheria haraka iwezekanavyo.

Sheria hii inaelekeza kuwa, Jeshi la Polisi au Magereza kuweka utaratibu utakaowezesha watoa msaada wa kisheria kutoa msaada wa huo kwa watuhumiwa na wafungwa kwa mujibu wa kanuni za sheria hii.

### 7.0 MASHARTI MENGINEYO

Wakili anayetoa msaada wa kisheria anapaswa kuzingatia kanuni za maadili ya uwakili. Hata hivyo, waziri amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni za maadili mema kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria zitakazozingatia mambo yafuatayo.

- i) Ulinzi wa haki na mslahi ya mtu anayepatiwa msaada wa kisheria;
- ii) Wajibu wa anayepatiwa msaada wa kisheria, msajili na mahakama;
- iii) Mgongano wa kimaslahi;
- iv) Kuzingatia usiri;
- v) Kwa *Wataalamu*, watapaswa kuzingatia kanuni za maadili ya taaluma yao; na
- vi) Zisizobagua

Pia endapo Wakili ataenenda kinyume na miiko ama maadili ya Uwakili kiasi cha kuathiri utoaji wa haki, basi, Jaji atatoa amri stahiki kwa mujibu wa haki na kwa maslahi ya mtu anayesaidiwa msaada wa kisheria.

Si ruhusa kwa mtoa msaada wa kisheria, wakili, mwanasheria au msaidizi wa kisheria kuonesha ubaguzi kwa mtu anayehitaji msaada kisheria kwa vigezo vya udini, jinsia, rangi , kabila au chama. Endapo mtoa msaada wa kisheria atafanya ubaguzi uliotajwa atakuwa anatenda kosa na akikutwa na hatia, atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi au kwenda jela si chini ya miezi sita na isiyozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Sheria hii pia imetoa adhabu kwa makosa ya jumla kama ifuatavyo;

- a) Kwa udanganyifu, atasababisha au kuruhusu taarifa za uongo kuingizwa katika rejista
- b) Atatoa msaada wa kisheria bila kuwa na sifa kwa mujibu wa sheria hii na/au atajifanya mtu aliyesajiliwa kwa mujibu wa sheria ya msaada wa kisheria
- c) Atatoa maelezo ya upotoshaji kwa ajili ya kujipatia faida au tija kwa mujibu wa sheria hii
- d) Atashindwa au kutakataa bila sababu ya msingi kuitikia wito mbele ya msajili
- e) Atazuia au kuingilia mjumbe wa Bodi, Msajili au mtu yeyote kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii;

Kwa hayo hapo juu atakuwa anafanya kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita jela au vyote kwa pamoja.

Kutakuwa na rejista ya watoa huduma wa msaada wa kisheria. Msajili atatangaza kila mwaka orodha ya majina ya watoa huduma waliosajiliwa na wale waliofutiwa usajili. Orodha hii ya majina itatangazwa kwenye gazeti la serikali au gazeti linalosambazwa sehemu mbalimbali na kusomwa na wengi au njia nyingine yoyote ya mawasiliano inayofaa.

Sheria inampa mamlaka waziri wa katiba na sheria kutengeneza kanuni za utekelezaji wa sheria hii. Pia sheria hii inafuta sheria ya msaada wa sheria (Mwenendo wa Makosa ya jinai) Sura ya 21. Bila kuathiri masharti ya sheria hii amri zote, kanuni, miongozo, na maagizo yaliyofanywa chini ya sheria iliyofutwa yataendelea kuwa na nguvu ya kisheria hadi pale kanuni mpya zitakapotengenezwa na kuanza kutumika rasmi.

Sheria hii ina jedwali linalotoa masharti ya utekelezaji, uundaji wa bodi, kipindi cha ukomo wa kuwa madarakani na taratibu za kuendesha vikao vya Bodi ya Taifa ushauri wa huduma za msaada wa sheria.

## **8.0 HITIMISHO**

Kijarida hiki kimebeba maudhui yaliyomo kwenye sheria ya Msaada wa Sheria, 2017. Kimechambua kwa lugha rahisi maudhui ya masharti yatokanayo na sheria hii ili kuweza kumsaidia mtu anayehitaji msaada wa kisheria na mtoa huduma ya msaada wa kisheria popote pale Tanzania. Kijarida hiki kitatumika na wadau wote katika tasnia ya sheria na msaada wa kisheria katika upatikanaji wa haki Tanzania. Pia kijarida hiki kinatoa mwongozo wa sifa za mtoa huduma za msaada wa kisheria na kinaeleza ni wapi huduma hii inaweza kupatikana. Haki na wajibu wa mtoa huduma na mtu anayehitaji msaada wa kisheria zimeelezwa vyema kwa kutazama mipaka ya kila upande katika upatikanaji wa haki nchini.

Kijarida hiki kitakuwa nyenzo muhimu kwa wasaidizi wa kisheria ambao kwa mara ya kwanza wanatambulika katika sheria hapa nchini, hivyo TANLAP inaamini maudhui yaliyoandikwa kwa lugha nyepesi katika kijarida hiki yataongeza tija ya kazi zinazofanywa na wasaidizi wa kisheria na watoa huduma za msaada wa kisheria hapa Tanzania. Pia kitawawezesha watu wasio na uwezo kupata haki kwa misingi sawa na watu wengine wenye kipato fedha.



